

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na: 025-2802318/2802137
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH BILIONI 2.9 ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE MPYA ZA SEKONDARI ZA KATA KUPITIA MRADI WA SEQUIP

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inatoa taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs 2,915,900,140 /= kutoka Serikali Kuu ikiwa ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule mpya za sekondari za Kata Mkoani Rukwa kupitia mradi wa SEQUIP. Fedha hizo ni kwa ajili ya miradi katika Kata ya Chanji Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Kata ya Mpombwe Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Kata ya Kalumbaleza Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Kata ya Ntatumbila Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na Kata ya Ninde Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Fedha hizo zitatumika kujenga Shule mpya za Sekondari katika Kata ambazo hazikuwa na Shule za Sekondari. Majengo yatakayojengwa kwa kila shule ni vyumba vya madarasa 8, Jengo la Utawala, Maktaba, Chumba cha TEHAMA na matundu ya vyoo 8, Maabara 3 (Fizikia, kemia na Bailojia), Kichomea taka na tanki la kuhifadhi maji safi.

Utekelezaji wa Mradi wa SEQUIP unatarajia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na hali inayotarajiwa kuongeza kiwango cha ufaulu. Mkoa wa Rukwa unaendela kuishukuru Serikali ya awamu ya Sita kwa kuendelea kuleta fedha za miradi ya maendeleo na kuboresha maisha ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa

Imetolewa na

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Khadija Dalasia'.

Khadija Dalasia

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Mkoa wa Rukwa

13 Julai 2023